

KUPENDANA

Darasa la 3
la watoto

by Denis & Devis Julius



MADARASA YA WATOTO

Haya ni mafundisho maalumu kwa watoto wenyewe umri wa miaka 0-12. Ni madarasa mbalimbali ambayo wewe kama mzazi/ mlezi/ mwalimu yatakusaidia kumwongoza na kumwandaa mtoto katika ukuaji bora wa kiroho. Hili ni darasa la Tatu (3), lkiwa hujapata miongozo ya nyuma basi utawasiliana nasi kwa namba zetu hizi bure, tuweze kukusaidia +255693036618/ +255789001312.

Bwana akubariki.

Mithali 22:6 Mlee mtoto katika njia impasayo, Naye hataiacha, hata ataka pokuwa mzee.

~Mchungaji Denis & Devis Julius.

Darasa la Tatu (3)

FUNDISHO KUU: KUPENDANA SISI KWA SISI.

Mstari wa agizo hilo: Yohana 13:34 Amri mpya nawapa, Mpendane. Kama vile nilivyowapenda ninyi, nanyi mpendane vivyo hivyo. 35 Hivyo watu wote watatambua ya kuwa ninyi mmekuwa wanafunzi wangu, mkiwa na upendo ninyi kwa ninyi.

Hatua ya kwanza (I):

Kabla ya kuwapa mfano wa kibiblia, mwalimu atawapima kwanza ufahamu wao juu ya upendo kwa kuwaauliza maswali haya;

Mwl: I) Upendo ni nini?, II) Je! Tunaonyeshaje upendo kwa wengine?

Ili kuwarahisishia ujibuji mzuri wa maswali hayo ni vema akatumia lugha ya picha, mfano [picha ya mtu anamkumbatia mwenzake, au mtu anamwinua mwenzake, au anampa mwenzake chakula n.k.] Na kuwaauliza kati ya hao ni yupi aliyeonyesha upendo kwa mwenzake? Na hapo Bila shaka Kila mmoja ataonyesha chaguo lake.



Hatua ya pili (2):

Habari ya Msamaria mwema. (Luka 10:25-37)

Hapa mwalimu, ataanza sasa kuwasimulia ile habari ya msamaria mwema iliyopo katika biblia, kwa lugha rahisi ya kueleweka kwa watoto, kabla ya kuwasomea moja kwa moja kutoka kwenye biblia. Vilevile itapendeza akitumia lugha za picha katika kila hatua ya simulizi hiyo.

Mwl:

“Mtu mmoja alikuwa anapita njiani, kwa bahati mbaya akavamiwa na wahalifu, wakamjeruhi, na kumvua nguo, na kumwacha karibu na kufa.

Kuhani mmoja (kiongozi wao wa kidini) akapita njia ile, lakini alipomwona akapita kando.

Baada kidogo, Mlawi naye (mwana-nchi mwenzake) alipita njia ile, naye pia alipomwona akapita kando

Mwisho akapita mtu wa taifa lingine (Msamaria), ambaye hakupendwa hata na taifa lao. Akamhurumia, kwa kumpa huduma ya kwanza na kumpeleka kwenye nyumba za wageni kwa ajili ya matunzo na huduma.

Ndipo Yesu aksauliza, katika ya hao watatu ni nani aliye jirani yake, Yule aliyeangukia kwa wahalifu?

Akajibu: Ni Yule aliyemwonea huruma.

Yesu akajibu: Nenda zako nawe ukafanye vivyo hivyo”



Hatua ya tatu (3):

Igizo:

Waaandae ingizo linaloendana na habari hiyo. (labda mmoja anaigiza kama kuhani, mwingine mlawi, wengine wachache wahalifu, wanakwenda kumvamia Yule mtu mwema.)

Baada ya igizo hilo, Waulize kati ya hao ni nani aliyeonyesha upendo? Na Bila shaka watakujibu ni Yule aliyesimama kama msamaria.

Hatua ya nne (4):

Maswali:

Mwl: Waulize kwanini wanadhani, Mlawi na Kuhani hawakumsaidia?
[Kila mtoto atatoa mapendekezo yake]

Mwl: Baada ya kutoa maoni yao, utawasaidia sababu kuu kama hizi:
Huwenda Walijiona wana shughuli za muhimu za kufanya zaidi ya kumsaidia, huwenda walikwepa gharma, huwenda walimdharau na kumwona kama mtu asiyeweza kuwasaidia kwa chochote, hata baada ya kumsaidia, n.k..

Mwl: Je ni nani tunapaswa tumwonyeshe upendo. Ni ndugu zetu tu wenyewe?

Watoto: Hapana, bali hata kwa watu wa mbali.

Hatua ya Tano (5):

Upendo kimatendo:

Wasomee sasa habari hiyo kwenye biblia, pia wasimamie wakariri mahali ambapo habari hiyo inapatikana (Luka 10:25-37). Hiyo itawasaidia kuhifadhi kumbukumbu njema katika usomaji wao baadaye.

Baada ya hapo, wagawie majukumu ya kwenda kufanya nyumbani, kwamfano unaweza kutengeneza vikaratasi vingi, ukaandika matendo mbalimbali ya upendo, kisha ukawaagiza wakatendee kazi na kipindi kijacho watakachokutanika, kila mmoja atasimulia ni nini amekifanya sawasawa na alichoelekezwa. Kwamfano kikaratasi kimoja utaandika kamsaidie mwanafunzi wenzako kufua soksi za shule, nyingine kampatie pipi/biskuti mtoto mwenzako, nyingine kamsaidie kufagia nyumbani, kamkumbatie, kamwombee, kambebe daftari lake la Sunday school n.k. kila mmoja akafanye cha kwake.

Hatua ya sita (6)

MAOMBI:

Wafundishe kusali sala hii fupi;

Watoto: “*Bwana Yesu asante kwa kutufundisha upendo, ni maombi yetu utuongzee moyo wa kupendana kwa dhati kama wewe ulivyotupenda sisi, upendo ambao tutauonyesha hata kwa wale ambao si ndugu zetu*”.

Wimbo: Wafundishe wimbo mzuri wenyе maudhui ya upendo wa sisi kwa sisi au wa Mungu kwetu, kisha wauimbe. Mfano wa Tenzi za rohoni (Mungu ni pendo – Tenzi no.27, ni wimbo mzuri wa kuwafaa.)

Mwisho:

Wapewe nafasi ya kukiwasilisha kile walichojifunza mbele kanisa/ jamii ya watu. Kwasababu sio tu itawajengea ujasiri wa kiroho, lakini pia itawahubiria injili wengine.

Bwana akubariki.

Mawasiliano.

Huduma ya Nuru ya Upendo wa Kristo.

www.wingulamashahidi.org

+255789001312/ +255693036618

info@wingulamashahidi.org